

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

18/12/2018

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MAELFU WAJITokeza KUTUMIA FURSA YA WAZIRI LUKUVI NA RC MAKONDA YA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI.

Maelfu ya wakazi wa Wilaya ya Ilala leo wamejitokeza kwa wingi kuitika wito wa Mkuu wa Mkoa huo Mhe. Paul Makonda wa utatuzi wa migogoro ya ardhi ambapo wamepongeza kuona migogoro yao ambayo mingine ni sugu inapatiwa ufumbuzi na majibu ya papo kwa papo.

RC Makonda amesema mkoa huo umeamua kufunga mwaka kwa kusikiliza kero za migogoro ya ardhi na utoaji wa hati za makazi ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na uhakika wa makazi.

Aidha RC Makonda amesema shauku yake ni kuona maeneo yote ya jiji la Dar es salaam yanapimwa na wananchi kupatiwa hati za makazi ili kupunguza migogoro ya viwanja, mashamba, mipaka, fidia na utapeli wa watu kuuziwa eneo moja zaidi ya watu wawili jambo linaloleta usumbufu kwa wananchi.

Ziara hiyo ya siku tano za utatuzi wa migogoro imeanza rasmi leo chini ya usimamizi thabiti wa Waziri wa Ardhi Mhe. William Lukuvi na RC. Makonda inalenga kupunguza migogoro ya ardhi iliyowasumbua wananchi kwa muda mrefu.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

